



Press Release  
Communiqué de Presse  
Taarifa kwa waandishi wa habari  
ICC-CPI-20070129-196

## Chumba cha utangulizi I chamtuma sheriani bwana Thomas Lubanga Dyilo

The Hague, tarehe 29 Januari 2007

Hali: Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo

Kesi : Mwendesha mashtaka dhidi ya Thomas Lubanga Dyilo

Chumba cha utangulizi I cha Mahakama ya Kimataifa ya jinai kimehakikisha mashtaka matatu ya Mwendesha mashtaka dhidi ya bwana Thomas Lubanga Dyilo yanayohusu muda uanaoanzia Septemba 2002, tarehe ya kuundwa kwa chama cha "Forces patriotiques pour la libération du Congo (FPLC) hadi tarehe 13 Agosti 2003. Chumba cha utangulizi I kimetuma kesi mbele ya Chumba cha kesi (*Trial Chamber*) ili kiamue. Wanamemba wa chumba hiki cha kesi watatangazwa na Ofisi ya Prezidenti wa Mahakama.

Uamzi wa Chumba cha utangulizi I ulifupishwa kwa mdomo na mwamuzi prezidenti Claude Jorda leo mjini The Hague kwenye mkusanyo wa kesi hadharani.

Chumba kiliamua kwamba kulikuwa ushuhuda wa kutosha unaobainisha sababu za msingi za kuamini kwamba bwana Thomas Lubanga Dyilo, ye ye kama mojawao wa wahalifu, alijihuisha na kupatikana na hatia kwa jinai za vitani ambazo ni kuwatia kwa nguvu kwenye jeshi na kuwaandikisha watoto wenyewe umri wa myaka chini ya kumi na tano katika FPLC, hii ikiwa tawi la kijeshi la "Union des patriotes congolais(UPC)", na kuwashirikisha kikamilifu kwa mapambano hapo Ituri (katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo), kwa muda unaoanzia Septemba 2002 hadi tarehe 13 Agosti 2003.

Chumba kiliona kwamba kuna sababu za msingi za kuamini kwamba kiisha kuundwa kwake, FPLC inadhaniwa kuwa ili andikisha watoto, na kuandikisha watoto jeshini ilikuwa zoezi na ilifahamika na rai Wahema pia lengo lake lilikuwa la kuhusisha watoto wengi. Kiliweka mkazo na kusema yakwamba kulikuwepo na ushuhuda wa kutosha unaobainisha sababu za msingi za kuamini kwamba kiisha mafunzo ya kijeshi, watoto walifikiriwa kuwa hodari kwa mapambano na pia makamanda wa FPLC tayari waliwaweka kwenyi mustari wa kwanza wa mapambano.

Chumba kilichukulia kwamba kulikuwa ushuhuda wa kutosha unaobainisha sababu za msingi za kuamini kwamba wakati wa kuundwa kwa FPLC, yaani mwanzo wa mwezi Septemba 2002, makubaliano ao mpango wa pamoja uliunganisha Thomas Lubanga Dyilo na makamanda wakuu wengine wa FPLC. Mpango huo anadhaniwa kuwa ulikuwa na lengo la kuimarisha jitahida za vita kwa kuwaandikisha vijana kwa utashi wao ao kwa nguvu katika vikosi vya FPLC, kwa kuwapatia wakurutu hao mafunzo ya kijeshi, kwa kuwashirikisha kikamilifu katika operesheni za kijeshi na kuwatumia kama magadi(*body-guard*). Chumba kilichukulia kwamba kulikuwa ushuhuda wa kutosha unaobainisha sababu za msingi za kuamini kwamba Thomas Lubanga Dyilo alikuwa na jukumu la muhimu la uratibu kwa jumla katika utekelezaji wa mpango wa pamoja, na alikuwa na majukumu mengine katita utekelezaji wa mpagno huo wa pamoja akijua pia karama ya majukumu aliyokuwa nayo.

Kulingana na Chumba cha utangulizi I, hata kama makubaliano ao mpango wa pamoja haukulenga wazi watoto wenyi umri chini ya myaka kumi na tano-uli dhamiria hakika vijana wakurutu kwa jumla –utekelezaji wake ungeweza lazma, kufutana na hali jirsi mambo yalivyokuwa yakiendelea, kuathiri watoto wenyi umri chini ya myaka kumi na tano. Chumba kilichukulia kwamba kulikuwa ushuhuda wa kutosha unaobainisha sababu za msingi za kuamini kwamba Thomas Lubanga Dyilo na makamanda wakuu wengine wa FPLC walielewa na kukubali pamoja matokeo hayo.

Habari za msingi kuhusu kesi ya *Mwendesha mashtaka dhidi ya Thomas Lubanga Dyilo* :

- Tarehe 10 Februari 2006, Chumba cha utangulizi I kili toa hati ya kukamata dhidi ya Thomas Lubanga Dyilo;
- Tarehe 17 Machi 2006, Thomas Lubanga Dyilo alipelekwa kwenye kituo cha zuizi cha Mahakama pa The Hague;
- Tarehe 20 Machi 2006, Thomas Lubanga Dyilo alifikishwa kwa mara ya kwanza mahakamani mbele ya Chumba cha utangulizi I;
- Chumba cha utangulizi I kinaundwa na muamuzi prezidenti Claude Jorda(Ufaransa) na waamuzi Akua Kuonyehia(Ghana) na Sylvia Steiner(Brazili).
- Wakati wa mkusanyo wa kesi wa kuhakikisha mashtaka uliofanyika tangu tarehe 9 hadi tarehe 28 Novemba 2006, Chumba cha utangulizi I kilisikiliza hoja za pande zote na maoni ya wawakilishi kisheria wa wateswa.

---

Kwa maelezo zaidi, tafadhalii uhusiane na :

Ofisi ya habari kwa umma ya Mahakama ya Kimataifa ya jinai, Sonia Robla, Mkuu wa Tawi, +31 (0) 70 515-8089 ao sonia.robla@icc-cpi.int

Ofisi ya habari kwa umma ya Mahakama ya kimataifa ya jinai, Paul Madidi, Mratibu katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo,  
+31 (0)6 46 16 86 79, +243 99 80 11 403 ao paul.madidi@icc-cpi.int

Ofisi ya Mwendesha mashtaka wa Mahakama ya Kimataifa ya jinai, Florence Olara, Afisa wa mawasiliano - Habari kwa umma +31 (0)70 515 8723 ao florence.olara@icc-cpi.int

Wakili wa Utetezi, wakili Jean Flamme, +31 (0)70 515-9105 ao j.flamme@pandora.be

Wawakilishi kisheria wa wateswa, wakili Luc Walleyn, luc.walleyn@blanmailland.be

---